

Pambazuko

Toleo Namba 075

Jumatatu Juni 10-16, 2024



Msigwa kutimkia CCM

• *Yaelezwa ni suala
la muda tu*

UK.11



Jicho la Tai

**Ebo! Eti Rais Samia ndiyo
anamaliza dola (\$) UK. 5**

Ulaya, Benki ya Dunia
'kuadabisha' Tanzania

UK.
8



JISAJILI HAPA: Andika neno HABARI na tuma kwenye
namba hii ya WhatsApp - 0744 768263 kupata gazeti bure

Tahariri

Mhimili wa gazeti la umma, Pambazuko

GAZETI la Pambazuko linandelea kujenga heshima kwa kuwapa wasomaji wake habari ambazo zimefanyiwa kazi kwa kina.

Pambazuko limekuwa gazeti la mfano na rejea mahali pengi tangu kianzishwa kwake miaka miwili iliyopita na linaendelea kujiimarisha kitaaluma kadri inavyowezekana.

Ni kutokana na imani kutoka kwa wasomaji wake, tumeona ni vyema kuweka kwa umma misingi na imani za waandishi wa habari wa Pambazuko ili kila msomaji atambue kuwa watendaji wa Pambazuko wanasimama katika imani za namna gani.

Watu wengi wameuliza, je, Pambazuko ni gazeti kama magazeti mengine, mbona linaonekana kuwa tofauti na vyombo vingine, hasa katika

kuandika habari na kutaarifu umma?

Jibu la swali hili ni rahisi kwa maana kwamba waandishi wa habari wa Pambazuko wanasimamia imani 10 ambazo zimekuwa mwongozo wa utendaji wao wa kila siku.

Pamoja na kwamba gazeti hili husambazwa bure kwa njia ya WhasApp, ni chombo ambacho kimesajiliwa na kutambuliwa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kwamba linafuata na kuzingatia miiko yote ya uandishi wa habari na zaidi sana kuongeza weledi na umakini katika kufanya kazi zake.

Hivyo, ni chombo cha habari chenye hadhi sawa na magazeti, radio, vituo vya televisheni na vyombo vingine rasmi na vinavyotambulika.

*Mhariri Mkuu
Juni 9, 2023*

Imani 10 za mwandishi wa Pambazuko

1. Kwamba kufikiri na kuamua kwa uwazi, usahihi na kuandika habari kwa kuzingatia miiko ya uandishi wa habari ndiyo msingi wa kazi zangu.

2. Kwamba kamwe sitaandika habari za kutunga, uongo wala uzandiki kwa lengo la kudanganya jamii au kuumiza yeyote.

3. Kwamba nitahakikisha kinachopeleka kwa mhariri ni ukweli, tena ukweli mtupu.

4. Kwamba nitaweza kuitetea – kwa ushahidi, habari ambayo nitaandika hata ikiwa ni mahakamani.

5. Kwamba nitashiriki kuhakikisha matangazo, habari, makala, safu na hata barua za wasomaji zinazingatia miiko ya uandishi wa habari na kamwe hazina lengo lililojificha.

6. Kwamba ubora wa kazi zangu – kupitia Pambazuko, utapimwa kwa uadilifu, uaminifu na usahihi wa kile kinachochapisha.

7. Kwamba, kumcha Mungu ni chanzo cha maarifa na uandishi bora, elimu bora; darasani na chumba cha habari cha Pambazuko, ni sehemu muhimu kujiendeleza kitaaluma.

8. Kwamba sitaogopa kuandika ukweli, hata kama utaumiza baadhi ya watu. Lengo ni kuponya jamii pana.

9. Kwamba rushwa ni adui wa haki, sitatoa wala kupokea na nitaandika wanaojihusisha nayo ili kuokoa jamii.

10. Ninaamini kuwa uandishi bora wa habari siku zote unajali utu, kamwe sitabagua.

HALAFU IKAWAJE...?



Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, January Makamba (kulia) akiteta jambo na Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye wakati wa mkutano wa waandishi wa habari uliofanyika Ikulu, Dar es Salaam wiki iliyopita, Juni 6. (Picha na Ikulu).

Jisajili kupata Pambazuko bure

- Ndugu msomaji wetu, jisajili kwa namba hii ya simu ya **WhatsApp: +255 744 768263** kwa kutuma neno **“HABARI”** kwa namba yako ya WhatsApp ili kupata Pambazuko kwenye WhatsApp yako.

- Pia unaweza kujisajili kwa kutumia **Email hii: pambazuko.tza@gmail.com** ili gazeti la Pambazuko likufikie kupitia email yako, andika neno **“HABARI”** na kutuma kwetu nawe utakuwa umejisajili.

NUKUU



“Maisha ni kama kuendesha baiskeli, ili kuendelea mbele, ni lazima kuendelea kukanyaga pedeli kuifanya baiskeli isonge. Ukiacha kukanyaga, siyo tu baiskeli itasimama, bali itaanguka kabisa ” - Mwanafalsafa Albert Einstein

Tangazo

Tuchangie

Endapo utapata changamoto katika kutuma mchango wako na wale wengine tuliowaomba kuchagia, tafadhali wasiliana nasi kwa namba hii na utahudumiwa kwa furaha; **0744 768 263**

Mhariri Mkuu,
Oktoba, 2023

Changia Pambazuko liendelee

WAJUMBE wa Bodi ya Uhariri, Mhariri Mkuu, wahariri, waandishi na watendaji wote wa gazeti la Pambazuko wameendelea kufuraha kusambaza habari, makala, safu, maoni, picha kwa miezi 15 bure kwa wasomaji wake.

Katika kipindi chote hicho cha kusambaza habari bila malipo, watendaji wa Pambazuko wamekuwa wakituma fedha, muda, ujuzi na rasilimali zingine kuhakikisha kila Jumatatu, gazeti hili linawafikia zaidi ya watu 500,000 duniani kote, bila malipo.

Ikumbukwe kwamba wazungumzaji wa lugha adhimu ya Kiwahili duniani kote; wanalitumia gazeti hili siyo kwa kupata habari tu, bali hata kusambaza kwa wengine kujifunza lugha hiyo inayokuwa zaidi kwa sasa.

Katika kipindi cha uhai wa gazeti hili - miezi 15, mengi mazuri yamepatikana, mbali na kukua Kiwahili, kuhabarisha, kupaza maoni ya watu, lakini pia Pambazuko limeviza kusukuma watoto uamuzi, hasa serikali kuchukua hatua kwenye baadhi ya mambo ambayo yameweka wazi kwa umma. Gazeti hili limesaidia kuepusha majanga, kuponya majaraha na zaidi sana, kuunganisha jamii na kuchochea umoja na kumarisha amani.

Pamoja na mafanikio hayo makubwa - na bado yanaendelea, uongozi wa Pambazuko umepokea mawazo kwamba gazeti hili linazoe kusuzwa, lakini hasi kubaliana na mawazo ya idadi kubwa ya wasomaji wake wanaopendekeza gazeti hivyo.

Lakini, uongozi huo umekubaliana na mawazo ya wachache kuruhusu umma kuanza kuchangia fedha kwa hiari ili kutoa mwanya kwa gazeti hili kuendelea kuufikia umma bure.

Sasa basi, endapo utapata changamoto katika kutuma mchango na uhai wa Pambazuko, tafadhali tumia namba hizi kwa ajili ya mchango wako wa fedha.

Unaweza kutuma mchango wako na kuhimiza wengine kufanya hivyo kwa kuanzia shilingi 1,000 na hakuna ukomo wa kiwango cha juu; chochote kinapokelewa kwa shukrani na hakika tutatambua mchango wako. Kwetu sisi, hatuna kikubwa wala kidogo; yote ni mchango na ina thamani sava ya "asante" kutoka kwetu.

Tuma mchango wako kutoka mtandao wowote wa simu yako ya mkononi - kwenda namba hii ya Lipa kwa TIGO na utatufikia; 6214500, Pia unaweza kuchangia kupitia namba ya Mpesa: 0744 768 263

Ukituma mchango wako kupitia simu, hakikisha jina linaandali: **Pambazuko Gazeti**. Endapo utapata changamoto katika kutuma mchango wako - na wale wengine uliowaomba kuchagia, tafadhali wasiliana nasi kwa namba hii na utahudumiwa kwa furaha; **0744 768 263**.

Lipa kwa Simu

Lipa kwa kuscanner



Lipa kwa Namba

6 2 1 4 5 0 0

PAMBAZUKO GAZETI



Ebo! Eti Rais Samia ndiyo anamaliza dola (\$)

Na Igo AI

“SIJUI Watanzania ni watu namna gani?

Hawana jema hawa watu. Wao baya wanalaumu sana, zuri wanalaumu sana pia...

...Wakipewa mkate wanaomba kuwekea jibini, wakipewa vyote wanaomba kisu na uma ili wafaidi zaidi utamu wa staftahi yao, wakijidai wazungu...

... Ni Watanzania haohao, wakipewa sharubati wanatamani yenye ubaridi. Wakipewa ya uvuguvugu, wanalaumu kwamba sharubati kamwe siyo chai...

Haya yalikuwa maneno aliyoamka nayo Mzee Tai leo asubuhi. Hata bila salamu kaanza “kubwabwaja”- waliokuwemo ndani ya nyumba yake wakajua leo “kimenuka” – kama wanavyosema vijana wa mjini.

Kumbe bhana, Mzee Tai alivurugwa tangu jana usiku baada ya kutoka kwenye kijiwe cha kahawa – kwa rafiki yake Shayo, ambako alikutana na marafiki zake wa zamani na hata vijana wa sasa wanaopenda kwenda hapo kunywa kahawa na kupata yanayojiri hapa na pale.

Inavyoelekea Mzee Tai alilala na jambo zito na hakutaka kuliongelea usiku ule baada ya kurejea. Kijana wake anaeleza kuwa mzee hakula hata chakula alichoadaliwa mezani. Alilala akiwa na njaa yake.

Kitu cha ajabu, hakuomba hata kuchemshiwa maji ya kuoga, maana ana kawaida ya kuomba apate kuoga maji ya moto kabla hajajitupa kitandani kwake kulala.

Baadaye iligundulika kuwa Mzee Tai akiwa kijiweni pale, alisikia watu wakizogoa, eti Mama Samia, huyu kiongozi wa Tanzania na ‘chealedi’ wa chama tawala – CCM, ndiye anamaliza dola za Marekani kwenye benki zetu.

Kwamba safari za mara kwa mara za Mama, ndiyo “zinakomba” dola zooteee, kwani huko anakosafiri, kila hatua



Dola

anayopiga, inahitaji dola za taifa kubwa la Marekani.

Eti kwamba Mama anapojiandaa kusafiri nje ya nchi, ambako hufuatana na wasaidizi wake, huagiza Benki Kuu ya Tanzania (ikiitwa Bioti) kukusanya dola zotee na kumpatia.

Kwamba kukomba dola zoteee, ndiyo hasa sababu kubwa ya kukosekana kwa sarafu hizo za taifa kubwa la Marekani.

“Hawa watu wa ajabu sana, siendi tena kwenye kijiwe cha wajinga, yaani hawaelewi kabisa sababu za kukosekana kwa dola hadi wamsingizie Mama...

... Hivi hawajui kuwa Tanzania sasa haiuzi sana bidhaa na hata mazao nje ya nchi, ambako biashara hiyo husaidia kukusanya dola za Marekani kuja nchini...

... Hawa watu wa ajabu sana, sijui hata wamesoma wapi, hawajui dunia inavyokwenda, yaani uvivu wetu wa kufanya biashara kwa dola ndiyo tunampachika Mama tuhama tu zisizokuwa na chembe ya ukweli,” aliendelea kulalama Mzee Tai.

Mzee Tai akaomba atengenezewe kahawa yake nyumbani kuanzia leo na hataki tena kwenda kijiweni ambako alikuwa mpenzi mkubwa na miongoni mwa wazee wanaoheshimika.

Tafakuri

‘Kushindwa’ kwa ANC ni funzo au tangazo?

Na Dkt. Benson BAGONZA

UCHAGUZI Mkuu wa Afrika Kusini umekamilika. Chama tawala cha ANC kimeambulia asilimia 40 ya kura zote. Kimekuwa madarakani kwa miaka 30.

Hakika, huu siyo ushindi kwa sababu kuu mbili; ANC haiwezi kuunda serikali peke yake. Inabidi iviombe vyama vingine ili kuunda serikali. Na pia, vyama vingine kwa pamoja, vina kura nyingi kuliko ANC (yaani asilimia 60).

Kwa hiyo, vyama hivi vinaweza kuungana na kuunda serikali ndani au nje ya bunge. Kwangu mimi, uchaguzi wa Afrika Kusini ni funzo na tangazo wakati huohuo.

Kwamba ANC imepoteza uwezo wake wa kujisahihisha kwa ndani. Macho yake hayaoni jipya kama wakosoaji wake wa nje wasivyoona jipya kwa ANC.

Ileweke kuwa kifo cha mbwa huanza kwa kupoteza uwezo wa kunusa hatari. Mbwa asiyenusu hatari au mawindo siyo mbwa tena! Hili ni tangazo.

Kwamba ANC imemkaribisha Julius Malema na chama chake cha EFF ili ashirikiane nayo kuunda serikali. Kumbe katika uhasimu wa kisiasa ni bora kuweka akiba.

Kumbe inawezekana chama fulani siku moja kumkaribisha Tundu Lissu, Freeman Mbowe na Zitto Kabwe kuunda serikali. Hili ni funzo.

Kwamba ANC na chama cha Democratic Alliance (chama cha makaburu wa zamani), wameanza mazungumzo ya kushirikiana kuunda serikali. Ukaburu wa zamani hautishi kuliko kukosa kuongoza serikali. Hili ni funzo na tangazo.

Kwamba chama cha Malema (EFF) kilikuwa kinatisha majukwaani na bungeni. Matokeo ya kura zake hayatishi. Kwa nini? Shetani amejificha katika sera zake za “mihemuko” (utaifishaji wa njia



Rais wa Afrika Kusini - Cyril Ramaphosa

za uchumi na ruhusa ya Waafrika wote kuingia Afrika Kusini). Kuna wakati wafungwa wanaweza kugomea msamaha. Hili ni funzo.

Kwamba anguko la ANC limetokana na uzee, rushwa, umaskini, kukosekana kwa ajira, na kukosekana kwa agenda inayowaunganisha Waafrika. Wakati mwingine ni bora kuwa na sera mbovu kuliko kutokuwa na sera. Hili funzo na tangazo.

Kwamba chama cha makaburu wa zamani (DA) kimepata ushindi wa pili. Siri ya ushindi wao? Hawana aibu na mambo yao, sera zao za soko huria zinaweka ugali mezani na kukwama kwa ANC kunawanufaisha. Shetani anayetimiza ahadi ana nafuu kuliko malaika mwenye ahadi tamu zisizotimizwa. Hili ni funzo.

Kwamba Chama cha MK (Umkhoto Wesizwe) kinachoongozwa na Jacob Zuma (Rais wa zamani wa Afrika Kusini), kimepata nafasi ya tatu. Hiki ni chama cha hasira kwa ANC, DA na EFF.

Hasira yao imelipa. Vyama vyote vinaogopa kuungana na MK kwa sababu ya historia. Zuma kama Donald Trump (Rais wa zamani wa Marekani)! Ogopa

‘Kushindwa’ kwa ANC

Inatoka Uk. 6

kiongozi aliye na “connection” na hitaji la watu hata kama ni la kipumbavu. Hili ni funzo.

Kwamba ANC haikujiandaa kugawana madaraka na yeyote. “U-milele” wa bandia uliitia upofu. Serikali itakayoundwa haitadumu kwa sababu ni hitaji la dharula.

Uongozi imara ni kujiandaa kwa yasiyotegemewa kuliko kujiandaa kwa yanayotegemewa. Hekima aliye juu siyo kuvuta ngazi alizopandia na kukaa nazo juu. Ni kuandaa godoro nene chini mahali pa kuangukia. Kesho inaandaliwa jana siyo leo. Hili ni funzo.

Kwamba ANC imegawanyika na kuzaa MK na EFF. Itagawanyika zaidi kwa kuwa kiunganishi kimedhoofika (madaraka).

Chama kisichogawanyika siyo chama halisi. Chama kinachoamini hakiwezi kugawanyika, kimeanza safari ya kugawanyika.

Hatuhitaji kuvigawa vyama kwa sababu vina uwezo wa kugawanyika vyenyewe. Viongozi siyo malaika na malaika siyo viongozi wa vyama. Hili ni funzo na Tangazo.

Mwandishi wa tafakuri hii ni Askofu wa Kanisa la Kilutheri la Kiinjili (KKKT), Jimbo la Karagwe. Ni mchangiaji wa makala Pambazuko.

Pambazuko

Tangazo

WANATAKIWA WAANDISHI WA HABARI

PAMBAZUKO ni gazeti la kibunifu la mtandaoni, linatolewa bure kila siku ya Jumatatu na kusambazwa kwa njia ya WhatsApp, Signal na Email.

Gazeti la Pambazuko linandelea kukua na kujiimarisha, hivyo kuhitaji maandishi wa habari ambao watasaidia kufikia malengo yake makubwa.

Waandishi wanaohitajika ni wale wenye uzoefu wa kuandika habari za uchunguzi, kufanya mahojiano mahsusi na wenye utayari wa kujifunza mambo makubwa yanayolenga kujenga taswira ya mhimili unaoaminiwa na umma.

Endapo unadhani unaweza kuwa miongoni mwa maandishi wa Pambazuko, tafadhali tuma maombi yako – ukiambatanisha na wasifu wako kupitia njia zifuatazo;

Email: info@pambazuko.or.tz. Simu (WhatsApp): 0754 768263

Mwisho wa kupokea maombi haya ni Juni 15, 2024.

Habari

Ulaya, Benki ya Dunia ‘kuadabisha’ Tanzania

Na Mwandishi WETU

KAMISHENI ya Ulaya (EC) imeungana na Benki ya Dunia kusitisha ufadhili wa miradi ya uhifadhi nchini Tanzania kutokana na madai ya ukiukwaji wa haki za binadamu.

Taarifa ilitolewa na The Maasai International Solidarity Alliance (MISA) inaeleza kuwa EC imeiondoa Tanzania katika orodha ya nchi za Afrika Mashariki ambazo zitanufaika na kiasi cha Euro milioni 18 (Shilingi bilioni 47) zitakazotolewa kama msaada kusaidia shughuli za uhifadhi katika eneo la Afrika Mashariki.

MISA ni shirika la kimataifa lisilo la kiserikali linalotetea haki za watu wa jamii ya Kimasai wanaoishi katika eneo la Hifadhi ya Ngorongoro na Loliondo, Tanzania.

Fedha hizo zimetengwa kama sehemu ya mradi ujulikao kama NaturAfrica.

“Uamuzi huu unatoa ujumbe mkubwa kwani unakuja kipindi kifupi tangu Benki ya Dunia nayo itangaze kusitisha kufadhili mradi wa kuendelea utalii katika kanda ya kusini (ikijulikana zaidi kwa jina na Regrow),” inasema taarifa ya MISA iliyotolewa mwishoni mwa wiki.

Aidha, hatua kama hiyo imeshachukuliwa na Shirika la Maendeleo la Ujerumani ambalo mwaka jana lilisitisha ufadhili wa miradi iliyokuwa inifadhili katika eneo la Loliondo.

Hatua ya kusitishwa kwa ufadhili wa EC inatokana na MISA kuwasiliana na taasisi kadhaa katika Jumuiya ya Ulaya (EU) na wanachama wake kuelezea matukio ya ukiukwaji wa haki za binadamu yanatodaiwa kufanywa na Tanzania katika maeneo hayo.

MISA inaituhumu Tanzania kwa kuwalenga watu wa jamii ya Kimasai katika operesheni nyingi zinazohusu uhifadhi na kuendeleza utalii kama kisingizio cha kuwahamisha kutoka kwenye maeneo waliyoishi kwa muda mrefu.



Rais Benki ya Dunia - Ajay Banga

Taasisi hiyo inadai kuwa serikali inatumia fedha inazopewa na wafadhili kuwanyanyasa wananchi wake.

“Kwa kutumia kisingizio cha uhifadhi, Tanzania inapokea mamilioni ya fedha ambazo inazielekeza katika eneo la kaskazini mwa nchi kwa lengo la kuanzisha “maeneo yanayolindwa”, kuendeleza shoroba za wanyama na kupanua mbuga za wanyama na maeneo ya hifadhi,” inasomeka sehemu ya taarifa hiyo.

Mwezi uliopita MISA iliandikia EC na kueleza kuziwasili wake iwapo fedha ilizopanga kuzitoea kwa ajili ya kuendelea uhifadhi Afrika Mashariki hazitatumiwa pia ‘kuwakandamiza’ wananchi katika maeneo yatakayofadhiliwa.

Taasisi hiyo iliieleza EC kuwa Tanzania ina rekodi ya kutoheshimu uamuzi wa mahakama na kutoa mifano kadhaa kthibitisha hilo.

Mwezi Aprili mwaka huu Benki ya Dunia ilitangaza kusitisha ufadhili wa mradi wa Regrow baada ya kupokea malalamiko kuhusu ukiukwaji wa haki za binadamu katika utekelezaji wa mradi huo.

Malalamiko hayo yaliwasilishwa kwa Benki ya Dunia na waathirika wa mradi huo kupitia taasisi ya Oakland Institute, wakiituhumu Tanzania kwa kutumia nguvu kubwa kuwahamisha watu



Hoja Yangu

Na Rashid MTAGALUKA

Samia sasa astahili tuzo ya Mo Ibrahim

Na Rashid MTAGALUKA

SOTE tunakubaliana kwamba tuzo ya Mo Ibrahim ilianzishwa mwaka 2007 na bilionea wa Sudan, Mohamed 'Mo' Ibrahim, kupitia taasisi yake kwa madhumuni ya kuwatuza viongozi wa Afrika, hasa marais na wakuu wa serikali walioonesha uongozi uliotukuka katika nchi zao.

Hadi sasa tuzo hiyo inayoendana na zawadi ya dola za Marekani milioni 5 imetolewa kwa marais saba tu; Joachim Chisano wa Msumbiji, Festus Mogae wa Botswana, Patros wa Cabo Verde, Hifikepunye Pohamba wa Namibia, Ellen Johnson wa Liberia, Mahamadou Issiofou wa Niger na Nelson Mandela aliyepewa kwa heshima.

Marais hawa walipewa tuzo hii kutokana na waliyoyafanya kwa wananchi wao, kuanzia utawala bora mpaka maendeleo endelevu katika nchi husika. Ingawa sasa ni miaka mitatu tu sasa, lakini Rais Samia Suluhu Hassan naye ameweka alama kubwa katika uongozi wake kwa kuwatumikia vyema wananchi.

Ni juhudi zake na kuwajibika ndiko kumemfanya apate shahada kadhaa za heshima kutoka vyyuo vikuu mbalimbali.

Kimsingi, shahada hizo kutoka vyyuo vikuu vinavyoheshimika duniani, "hazitolewi kama karanga," bali kuna vigezo vyake vingi, tena vikitazamwa na kuchunguzwa kwa makini kabla ya kupatiwa mhusika.

Mo Ibrahim Foundation inatoa tuzo kwa Uongozi Bora Afrika, inayolenga kuwatambua na kuwatuza viongozi wa bara hilo walioweke mfano mzuri katika uongozi na maendeleo ya nchi zao.

Rais Samia ameonyesha uongozi bora na kujitolea kwake katika kuboresha uhusiano na tasnia ya habari, jambo



Rais Samia Suluhu Hassan

linaloweza kumuweka katika nafasi nzuri ya kushinda tuzo hii.

Rais Samia ameweka rekodi ya kusafiri na waandishi wa habari katika ziara zake za ndani na nje ya nchi, hatua inayoongeza uwazi na kuruhusu vyombo vya habari kufikia taarifa za moja kwa moja kuhusu shughuli za serikali.

Utambuzi wa kimataifa

Shahada za heshima alizotunukiwa Rais Samia kutoka taasisi mbalimbali za kimataifa ni ishara ya kutambuliwa kwake kimataifa kwa uongozi bora.

Hoja yangu ni kwamba, heshima hizi zinathibitisha juhudi zake katika kuboresha elimu, afya, na maendeleo ya kiuchumi na kijamii nchini Tanzania.

Hivyo, kamati inayoratibu tuzo hizo iangalie upya kama kuweka kigezo cha uhusiano na tasnia ya habari katika tuzo ya Mo Ibrahim kinaweza kuwa kipimo kizuri cha uongozi bora.

Kutokana na mafanikio yake katika uongozi, kutambuliwa kimataifa kupitia shahada za heshima, na juhudi zake za kuimarisha tasnia ya habari hapa nchini, Rais Samia Suluhu Hassan ana nafasi kubwa ya kutunukiwa Tuzo ya Mo Ibrahim.

Rashid Mtagaluka ni mwandishi wa habari na anapatikana kwa simu nambari 0784 438 546/ email; mtagaluka@gmail.com

Nigeria

Utawala wa Tinubu, mwiba kwa waandishi

UTAWALA wa Rais Bola Tinubu wa Nigeria unatajwa kuwa mwiba kwa waandishi wa habari, kutokana na kuongezeka kwa matukio ya kuwakamata na kuwasweka ndani wanahabari nchini humo.

Tukio la hivi karibuni la kukamatwa kwa mwanahabari Daniel Ojukwu jijini Lagos, limeibua sintofahamu kwa wanahabari nchini humo, likifanywa na maofisa wa Jeshi la Polisi.

Jarida la The Continent linaandika kuwa akiwa mjini Lagos, Ojukwu, mwandishi wa habari za uchunguzi alikamatwa na askari polisi watano wenye silaha ambao wameelezwa kutokea Abuja.

Akiwa katika Idara ya Upelelezi wa Makosa ya Jinai jijini Lagos, Ojukwu alionekana akiwa amefungwa pingu huku mikono yake ikibanwa kwa nyuma na kunyang'aywa kila alichokuwa nacho, huku akizuiwa kuwasiliana na mtu yeyote, akiwemo wakili wake na wanafamilia.

Alishikiliwa katika mahabusu kwa siku kadhaa bila kupata msaada wa kisheria wala kuonana na wanafamilia wake.

Hata baada ya wanafamilia na wafanyakazi wenzake kufanikiwa kujua alipo, polisi walimchukua na kumhamisha kutoka Abuja na kumpeleka katika kituo maalumu kinachoshughulika wahalifu wa mtandao mjini Abuja.

Alichiwa baada ya kukaa mahabusu kwa siku tisa, baada ya shirikizo kutoka kwa wanahabari wa Nigeria, vyama vya kiraia na Kamati Maalumu ya Kutetea Wanahabari yenye makao yake makuu nchini Marekani.

Ojukwu anakuwa mwandishi wa 45 kukamatwa tangu Rais Tinubu alipoingia madarakani Mei mwaka jana.

Kwa mujibu wa kiongozi wa mtandao unaoshughulikia haki na ulinzi wa wanahabari, Media Rights Agenda, Edetaen Ojo, karibu asilimia 62 ya



Daniel Ojukwu

ukamataji huu umefanywa na vikosi vya ulinzi vya serikali.

Haya yanafanyika hata baada ya Rais Tinubu kuahidi kulinda na kuheshimu uhuru wa wanahabari katika mkutano wake na wamiliki wa vyombo vya habari Desemba, mwaka jana.

Kwa mujibu wa ripoti ya Global Rights, rekodi ya Rais Tinubu inaonekana kuwa mbaya zaidi ya mtangulizi wake, Muhammadu Buhari ambaye utawala wake uliripotiwa kukamata hadi wanahabari 189 katika kipindi cha miaka minane.

Kituo cha kusimamia na kuendeleza waandishi wa habari nchini Nigeria kimeeleza kuwa kati ya mwaka 1986 hadi 2023, waandishi 1,034 wa Nigeria walikamatwa na kushikiliwa na vyombo vya ulinzi.

Hiyo inafanya idadi ya wanahabari 28 waliokamatwa katika kipindi kifupi cha utawala wa Rais Tinubu kuwa na uwiano mkubwa na ilivyokuwa katika tawala za kijeshi zilizopita kwa miaka 38.

•Makala haya ya uchambuzi, yamechapishwa kwa mara ya kwanza na The Continent, gazeti linalosambazwa kwa njia ya WhatsApp na kuchachapishwa kwa lugha ya Kiingereza. Unaweza kupata nakala yake bure, kila wiki kwa kujiandikisha kupitia namba hii: +27738056068

Msigwa kutimkia CCM

Na Elizabeth HOMBO

KUNA kila dalili kwamba aliyekuwa Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) Kanda ya Nyasa, Mchungaji Peter Msigwa akajiunga na Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Taarifa ambazo gazeti hili imezipata zinasema kuwa CCM tayari imesharusha ndoano kumshawishi mbunge huyo wa zamani wa Iringa Mjini kujiunga nacho.

Kwa muda mrefu sasa CCM imekuwa ikitamani kumpata mwanasiasa huyo machachari, lakini ikielezwa kuwa “hakuwa tayari kununulika,”

Hata hivyo, kwa fukuto la sasa la mnyukano wa mwenyekiti wake, Freeman Mbowe na Msigwa, huenda kinachosubiriwa ni siku chache tu kumuona Msigwa akiwa amevalia sare zenye rangi ya kijani, alama ya utambulisho wa CCM.

Inaelezwa kuwa wakati wa uongozi wa John Magfuli, rais wa awamu ya tano, Msigwa aligoma kupokea fedha na ushawishi wa nafasi za uongozi kama ilivyokuwa kwa baadhi ya wanasiasa waliokimbia kambi ya upinzani.

Sasa pamoja na ushawishi wa masuala kama hayohayo, kuna jambo jingine linalokoleza tetesi za Msigwa kuhamia CCM; ugomvi wa wazi kati yake na Mbowe.

“Tunasubiri muda tu, huyu mchungaji (Msigwa) ataunga juhudi, kwani hata nyie waandishi hamuoni namna mama (Rais Samia) anavyoitendea haki nchi yetu? Maisha yamekuwa murua, kuna amani tele na pesa zipo nje nje, labda kama ni mvivu,” kasema kiongozi mmoja wa CCM.

Huku akikataa kutajwa jina lake, kiongozi huyo amelieleza Pambazuko kwamba mazungumzo kati ya chama chake na Msigwa, yapo katika hatua



Mchungaji Peter Msigwa

nzuri.

Pambazuko limeelezwa kuwa CCM wanafanya hivyo wakiwa na lengo kubwa la kukidhoofisha Chadema ambacho katika siku za hivi karibuni kimekuwa kikitisa anga za kisiasa nchini kutokana na kuandaa maandamano na mikutano ya hadhara ambayo imevutia watu wengi.

Aidha, inaelezwa kuwa CCM inalenga kuwadhoofisha watu wanaotajwa kuwa wanaweza kuwania urais kupitia chama hicho kikubwa cha upinzani nchini katika uchaguzi mkuu unaotarajiwa kufanyika mwakani.

Tayari Katibu wa Halmashauri Kuu ya Taifa, Itikadi na Uenezi wa CCM, Amos Makalla, akiwa katika mkutano wa hadhara jijini Arusha Juni 3, 2024, alimpa pole Mchungaji

Msigwa kwa misukosuko anayopitia kwenye chama chake, huku akimkaribisha kujiunga na chama hicho tawala.

“Nimeona Msigwa akilalamika kutotendewa haki kwenye uchaguzi wa kanda ndani ya chama chake. Pole Mchungaji Msigwa, njoo CCM... kuna demokrasia tele, kuna uwazi. Huko upinzani hali siyo shwari na hicho chama hakikufai,” alisema Makalla.

Hata hivyo, alipotafutwa na

Habari**Msigwa kutimkia CCM***Inatoka Uk. 11*

Pambazuko, kupitia simu yake ya kiganjani ili aeleze kinagaubaga kuhusu ukweli wa taarifa hizo, Msigwa alisema kwa ufupi kuwa hana la kusema na kwamba waulizwe waliotoa taarifa hizo.

“No comment... sina la kusema kwa sababu sijui lolote labda uwarudie hao waliokueleza hizo taarifa wakwambie vizuri,” alisema Msigwa.

Tetesi za Msigwa kuhamia CCM zilianza kuibuka siku chache tu baada ya kushindwa na aliyekuwa Mbunge wa Mbeya Mjini, Joseph Mbilinyi (Sugu), katika uchaguzi wa mwenyekiti wa Kanda ya Nyasa.

Katika uchaguzi huo ambao uliofanyika Mei 29, 2024, mjini Makambako mkoani Njombe, Msigwa alikuwa akitetea nafasi hiyo ya uenyekiti wa kanda, lakini alishindwa mbele ya mpinzani wake, Sugu kwa tofauti ya kura mbili.

Akizungumza baada ya matokeo kutangazwa, Msigwa alisema ameyapokea matokeo hayo na anayeheshimu kwa sababu ni sauti ya wapiga kura.

Alisema kuwa yeye siyo mwaniasia ambaye haiba yake inajengwa na vyeo na kuwa nafasi za uongozi ni kitu cha kupita tu, hivyo hana shida yoyote baada ya kushindwa kwenye uchaguzi huo.

Siku chache kabla ya uchaguzi huo, akizungumza katika mdahalo ulioandaliwa na Star TV ya Mwanza ukimkutanisha na Sugu, Msigwa alieleza kuwa hatokuwa na shida kukubali matokeo na kumpongeza Sugu iwapo angemshinda katika uchaguzi huo.

Lakini, kwa mshangao wa wengi, siku chache baada ya kuangushwa katika uchaguzi huo aliitisha mkutano wa waandishi wa habari na kufanya kile ambacho alisema hawezi kukifanya, yaani kupinga matokeo.

Aliwambia waandishi wa habari kuwa hakubaliani na matokeo ya uchaguzi

*Mwenyekiti wa Chadema, Freeman Mbowe*

uliomweka Sugu madarakani kwa madai kuwa ulikuwa na kasoro nyingi.

Licha ya awali kutangaza kuwa vyeo siyo hulka yake, Msigwa aliwambia waandishi wa habari kuwa yeye siyp mtu wa kushindwa kwenye uchaguzi.

Bila kuwataja majina, Msigwa aliwatuhumu baadhi ya viongozi wa juu wa chama chake kupanga njama na mikakati iliyosababisha ashindwe katika uchaguzi huo.

Kisha akabainisha kuwa ameamua kukata rufaa katika ngazi husika akipinga matokeo ya uchaguzi huo.

Katika hilo, alieleza kuwa sababu za kuwasilisha rufaa ni kwa vile mifumo ya chama imetumika kumhujumu ili asishinde uchaguzi huo na kwamba uligubikwa na ukiukwaji wa taratibu na kuwepo kwa vitendo vya rushwa.

Pamoja na rushwa, Msigwa alisema baadhi wa wajumbe halali wa kikao cha Baraza la Uongozi la Kanda, walizuiwa kupiga kura kinyume na Ibara 5.2.1 ya Katiba ya Chadema.

“Nimekata rufaa kwa chama changu kuwa makatibu watatu wa mabaraza walizuiwa kupiga kura, ukiangalia kura zangu zilizoongezeka na kufikia sita, lakini wajumbe watatu walizuiwa.

“Rufaa yangu imefafanua mambo

Msigwa kutimkia CCM

Inatoka Uk. 12

mengi sana yaliyokiukwa katika uchaguzi hata kufutwa kwa uchaguzi wa Njombe, ulikuwa mkakati wa kunihujumu ili nisishinde. Lakini, nimegundua sikuwa nashindana na mpinzani wangu peke yake, bali alikuwa ana nguvu nyingine nyuma yake,” alidai Msigwa.

Mkurugenzi wa Uenezi na Mambo ya Nje wa Chadema, John Mrema, amethibitisha chama hicho kupokea rufani ya Msigwa na kuleza kuwa vikao husika vitakaa, kuijadili na kutoa majibu.

Ingawa Msigwa anaonekana kutoa hoja za kujenga uzito wa rufaa yake, lakini baadhi ya wachambuzi wanaamini kuwa anachokifanya kupitia hoja hizo, hasa pale anapowatuhumu viongozi wa juu wa chama na tasisi zake, ni sehemu ya hujuma ambayo amepanga kuifanya dhidi ya chama hicho kabla hajatimka.

Wachambuzi hao wanasema anachokifanya Msigwa hakina tofauti na kile kilichofanywa na aliyewahi kuwa mbunge wa viti maalum wa chama hicho, Upendo Peneza, ambaye mara baada ya kujiunga CCM akaanza kampeni kupitia vyombo vya habari akirusha tuhuma nzito dhidi ya viongozi na chama chake hicho cha zamani.



Joseph Mbilinyi - Sugu

“Msigwa anajua anachokifanya. Mtu hauwezi kuwa katika mtumbwi mnasafiri pamoja halafu uutoboe mtumbwi. Huyu kuna kitu anakilenga kwa sababu kama kweli angekuwa anabaki Chadema asingekubali kuona chama hicho kinadhoofishwa kwa kashfa kama hizi anazozisambaza,” kilisema chanzo chetu.

Hii siyo mara ya kwanza kwa hoja inayomhusu mwanasiasa huyo machachari kuhamia CCM.

Katika kipindi cha utawala wa serikali ya awamu ya tano chini ya John Magufuli (sasa marehemu), tetesi zilimhusisha Msigwa kuhamia CCM baada ya kupewa fedha nyingi, lakini akadai kuwa alizikataa.

Ulaya, Benki ya Dunia ‘kuadabisha’ Tanzania

Inatoka Uk. 8

21,000 ili kupanua mipaka ya mbuga ya wanyama.

Wananchi hao walituhumu kuwa zoezi hilo lilitawaliwa na matumizi ya nguvu kubwa, manyanyaso, vipigo na uharibifu wa mali zao bila kulipwa fidia stahiki.

Baada ya kupokea malalamiko hayo Benki ya Dunia ilituma timu ya kufanya uchunguzi wa awali ambayo ilitibitisha kuwepo kwa hali kama hiyo na kuifanya benki hiyo kufikia uamuzi wa kusitisha

ufadhili huo ili kufanya uchunguzi wa kina.

Benki ya Dunia ilikuwa imepanga kutumia kiasi cha dola za Marekani milioni 150 kufadhili mradi huo.

Hata hivyo, baada ya kutolewa taarifa za kusitishwa kwa ufadhili huo serikali ilisema kuwa uamuzi huo hautaathiri utekelezaji wa mradi, kwani hadi wakati huo kiasi kikubwa cha fedha kilikuwa kimeshatolewa.

Habari**Wakazi Mbozi wagoma kuhamishwa**

Na Mwandishi WETU,
Mbeya

WAKAZI wapatao 120 wa Kijiji cha Ndolezi, mkoa wa Songwe, wamegoma kuhamishwa kutoka kwenye eneo wanaloishi.

Wakazi hao wameenda mahakamani ambako wameishitaki serikali pamoja na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorogoro (NCAA) wakipinga kuhamishwa katika eneo hilo.

Kinachowatesa wananchi hao ni neema iliyopo kijijini hapo ambapo ndipo penye kimondo ambacho kwa miaka mingi kimekuwa kivutio kikubwa cha utalii.

Serikali kupitia NCAA inataka kuwahamisha wanavijiji hao ili kupata eneo kwa ajili ya upanuzi wa hifadhi kuzunguka kimondo hicho.

Lakini, wananchi hao wamekimbilia Mahakama Kuu Masijala ya Mbeya na kufungua kesi kupinga hatua hiyo ya serikali.

Wanatetewa na Wakili Philip Mwakilima, ambaye aliliambia Pambazuko wiki iliyopita kuwa mahakama imeipa serikali hadi Juni 12 mwaka huu iwe imewakilisha hoja kinzani dhidi ya hoja walizoziwasilisha kwa niaba ya wakajijiji hao.

“Wakazi wa Ndolezi wamefungua kesi hii wakipinga hatua ya serikali kupitia NCAA kutaka kuwahamisha kutoka kwenye eneo lao....

.... Tayari tumeshawasilisha hoja za kupinga hatua hiyo ya serikali. Sasa tunasubiri majibu kutoka kwao,” alisema wakili huyo nje ya mahakama baada ya kesi hiyo kuahirishwa Jumatano iliyopita.

“Serikali imetakiwa kuwasilisha majibu ya hoja zetu ifikapo Julai 12 na sisi, kwa niaba ya wanavijiji hawa, tumetakiwa kuwasilisha majibu ya hoja zao ifikapo Julai 19,” alifafanua wakili huyo.

Kesi hiyo imepangwa kutajwa tena Julai 10 mwaka huu.

Hoja kubwa ya wananchi hao katika kesi hiyo ni kuwa serikali bado haijalitangaza eneo hilo kama hifadhi ya taifa, hivyo kutokuwapo na msingi wa wao kuhamishwa kwa nguvu.

Inadaiwa kwamba kwa kuwa wanafahamu kuwa serikali ina nguvu wameamua kuchukua njia ya sheria kukabiliana na kile wanachoamini kuwa ni uonevu wa serikali dhidi yao.

Kinachofanywa na wananchi hao kinaweza kuwa kimetokana na masomo mawili makubwa.

Kwanza ni tukio lililotokea miaka miwili iliyopita ambapo Februari



Kimondo

Wakazi Mbozi wagoma kuhamishwa

Inatoka Uk. 14

2022 walijikuta wakipokea wageni wasiotarajiwa kijijini kwao.

Hawa walikuwa ni maofisa wa serikali walioambatana na askari wakiwataka kuondoka katika nyumba zao haraka kwa madai kuwa wanaishi eneo hilo kinyume cha sheria.

Katika tukio hilo baadhi ya watu walibomolewa nyumba zao, wengine wakapigwa na kupata manyanyaso kutoka kwa maofisa hao wa serikali na askari walioambatana nao.

Inaelezwa zaidi kuwa wananchi hao wameona kile kinachowatokea wakazi wenzao wa Ngorongoro ambao licha ya kuwapo kwa taarifa kuwa wanahamishwa kwa hiari, lakini kuna mazingira ambayo yanaonyesha kuwa kuhama huko siyo kwa hiari.

Baadhi ya wanavijiji hao, wakizungumza na Pambazuko nje ya mahakama hiyo walieleza kuwa kwa muda mrefu wamekuwa wakiishi kwa wasiwasi kutokana na vitisho kutoka kwa maofisa wa serikali kuhusu kuhamishwa katika eneo hilo ambalo wamekuwa wakiishi kwa miongo mingi.

“Nakumbuka kwenye lile tukio la mwaka 2022 baadhi ya wenzetu walifariki dunia kutokana na mshituko wa moyo kufuatia tukio lile. Wengi walishitushwa na mabomu yaliyokuwa yanapigwa na silaha nyingine za moto kwa sababu hatujayazoea mambo hayo,” anasimulia Raphael Cheyo.

Anaongeza, “hatutarudi nyuma kwa sababu sisi tunaamini eneo hili ni letu kihalali. Mababu zetu waliishi hapa kabla sisi hatujazaliwa. Hii ni ardhi yetu tangu mababu, inakuwaje leo aje mtu kutuambia kuwa tumevamia eneo hili!”

Mwaanakijiji mwingine, Ephrahim Maiyo alihoji; “Ina maana sisi wanakijiji hatuna haki? Kwa nini tuwekwe kwenye mazingira ya kuishi kwa hofu ndani ya nchi yetu wenyewe? Hatuwezi hata kufanya shughuli za maendeleo kwa amani.”



Wasiri wa Utalii - Angellah Kairuki

Mwaka 2022

Wakati watu wengine wakisherehekea sikukuu ya wapendanao Februari 14, 2022, serikali wilayani Mbozi ilituma maofisa wake wakiwa wameandamana na askari wa jeshi la polisi kwenda kuwahamisha wakazi wa kijiji hicho.

Katika zoezi hilo serikali ya wilaya ililenga kuwahamisha wakazi wapatao 1,300 kutoka katika kijiji hicho ili kuipa NCAA ardhi kwa ajili ya upanuzi wa Hifadhi ya Kimondo.

Hifadhi ya Kimondo, iliyopo katika kijiji cha Ndolezi, Kitongoji cha Isela, wilayani Mbozi, ipo chini ya NCAA ambayo inalenga kuipanua hifadhi hiyo kwa ajili ya kutenga eneo maalum ambalo wanyama mbalimbali watawekwa na hivyo kukifanya Kimondo cha Mbozi kuwa eneo la utalii kwa Mkoa wa Songwe.

Harakati za kutaka kuwahamisha wanakijiji hao zilianza mwaka 2020, lakini hazijafanikiwa hadi leo kwa sababu wananchi hao wamegoma kuondoka magali hapo.

Awali zoezi hilo lilipangwa kuwa la hiari, lakini baada ya wanakijiji kuonyesha kupinga, serikali ikaanza kutumia vitisho na nguvu dhidi ya wananchi hao.

Licha ya NCAA kuahidi kuwalipa fidia wananchi watakaohama kwa hiari, taarifa zinaonyesha kuwa zoezi hilo limekuwa likifanyika kwa lazima na kuwaletia usumbufu mkubwa wananchi hao wa Ndolezi.

Tangazo



Tangaza na **Pambazuko**

EWE mfanyabiashara na mtoa huduma, endapo unahitaji kuwafikia wateja wengi zaidi bila kujali mipaka ya eneo ulilopo, tangaza nasi

Pambazuko isaidie kupaisha na kupambazua huduma na biashara yako.

Kwa bei nafuu sana

0744 768 263 au
Barua- Pepe; info@pambazuko.tz

Yaliyotikisa uchumi mwaka wa fedha ukienda ukingoni

Na Mwandishi WETU

WAKATI Tanzania ikielekea ukingoni mwa mwaka wa fedha, taarifa zilizopo zinaonyesha kuwa uchumi wa Tanzania umefanya vizuri kwa mwaka 2023/24 licha ya changamoto lukuki zilizojitokeza.

Ripoti za Benki Kuu (BoT) zinaonyesha kuwa uchumi ulikua kwa wastani wa kati ya asilimia tano na sita kati ya Julai mwaka jana na na Machi mwaka huu.

Katika robo tatu ya mwaka 2023/24, BoT inabainisha kuwa uchumi ulikua kwa asilimia 4.6, huku sekta ya huduma ikionekana kufanya kazi vizuri zaidi.

Hata hivyo, pamoja na takwimu kuonyesha kuwa uchumi unafanya vizuri, lakini kuna changamoto nyingi ambazo zinakwaza ufanisi wa shughuli za wafanyabiashara na wananchi wa kawaida.

Kuadimika kwa sarafu la dola ya Marekani na kupanda kwa bei ya mafuta, ni kati ya changamoto ambazo zimeathiri ukuaji wa sekta ya biashara na sekta nyingine muhimu katika mwaka wa fedha unaomalizika.

Changamoto hizo zilisababisha kupanda kwa bei ya bidhaa nyingi na kufanya hali ya maisha kuwa mbaya miongoni mwa wananchi wengi wa kawaida.

Wafanyabiashara wengi wanaoagiza bidhaa nje ya nchi, walishindwa kuendesha shughuli zao vizuri kutokana na kuadimika kwa kwa dola ambayo kwa kiasi kikubwa ndio inatumika katika biashara vza kimataifa.

Serikali imekuwa ikieleza kila mara kuwa inachukua hatua kukabiliana na hali hiyo, lakini kadri siku zinavyokwenda hali ilizidi kuwa mbaya.

Ilifikia kipindi wafanyabisahawa walishindwa kuagiza bidhaa nje ya nchi



Wasiri wa Fedha - Dkt. Mwigulu Nchemba

kutokana na kuadimika kwa dola ya Marekani.

Hali hiyo imesababisha upungufu wa bidhaa ndani ya nchi na hivyo kuathiri bei kwa mlaji wa mwisho.

Pambazuko liliwahi kuripoti kuwa hali hiyo ililazimu Benki Kuu ya Tanzania (BoT) kulazimika kuingilia kati suala hilo.

Gavana wa BoT, Emmanuel Tutuba alisema kuwa tatizo hilo halitokana na mifumo ya kiuchumi au biashara ndani ya nchi.

Akasema kuna ugumu kwa nchi kuweka kando matumizi ya dola na kubainisha kuwa serikali kupitia BoT imekuwa ikichukua hatua mbalimbali kukabiliana na upungufu wa sarafu za kigeni.

Siyo Tanzania peke yake ndiyo iliathirika na hali hiyo, kwani mataifa mengine kama vile Ghana, Misri, Zimbabwe, Nigeria na Kenya, nazo ziliathirika pia.

Baadhi ya mataifa hayo yalianza kufukiria kuacha kutumia dola kama ambavyo baadhi ya wafanyabiashara

Habari**Yaliyotikisa uchumi mwaka
wa fedha ukienda ukingoni***Inatoka Uk. 17*

nchini nao wameanza kufikiria hivyo.

Wiki iliyopita baadhi ya wafanyabiashara walieleza kuwa wameamua sasa soko la dunia kutokana na sarafu ya Euro katika biashara zao za kimataifa, kwani upatikanaji wake siyo wa mashaka kama ilivyo kwa dola.

Bei ya mafuta

Kwa upande mwingine, uchumi uliyumbishwa na kupanda kwa bei ya mafuta katika dunia kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo vita kati ya Urusi na Ukraine.

Hali hiyo imefanya gharama za uzalishaji na usafirishaji nchini kuwa juu na hivyo kuathiri bei ya bidhaa na huduma.

Hata hivyo, wachambuzi wa masuala ya uchumi wamelieleza Pambazuko kuwa Tanzania ina nafasi ya kukabiliana na hilo kupitia kiwango kikubwa cha gesi asilia ambacho kimegundulika nchini.

Wamesema kinachotakia kwa sasa ni kuongeza kiasi cha matumizi ya gesi katika uzalishaji na usafirishaji.

Gharama za usafirishaji

Katika siku za hivi karibuni wakati bajeti ya mwaka 2023/24 ikielekea ukingoni, limebuka suala la ongezeko kubwa la gharama za usafirishaji wa bidhaa kutoka Mashariki ya Mbali na Ulaya.

Hali hiyo

inatokana na machafuko yanayoelendelea katika eneo la Mashariki ya Kati hasa vita baina ya Israel na kikundi cha Hamas cha nchini Palestina.

Vita hivyo vimezorotesha usalama katika maeneo ya ghuba kuzunguka Bahari ya Mediterranean ambayo ndiyo njia kuu ya bidhaa zinazoingia nchini kutoka ughaibuni.

Hilo limesababisha wasafirishaji kutumia muda mwingi kupitisha bidhaa Afrika Kusini au kutumia gharama kubwa kulipia bima ya bidhaa zinazosafirishwa baharini na hivyo kuongeza kwa kiasi kikubwa kwa gharama za usafirishaji.

Hesabu zilizotolewa hivi karibuni na wafanyabiashara wanaoagiza bidhaa kutoka China zinaonyesha kuwa kuna bei ya kusafirisha kontena moja kutoka china zimeongezeka kwa hadi asilimia 300.

Mvua za el-nino na umeme

Mvua za el-nino ambazo zilinyesha mwanzoni mwa mwaka huu zilisababisha uharibifu mkubwa wa miundiombinu kiasi cha kupandisha gharama za

Endelea Uk. 19

Muusa nyanya eneo la Ubungo, Dar es Salaam, Robison Mmasi, akieleza jambo wakati akhojiwa na gazeti hili kuhusu matarajio yake kwa Bajeti Kuu ya Mwaka 2024/205. (Picha na Fidelis Felix /Pambazuko).

Yaliyotikisa uchumi mwaka wa fedha ukienda ukingoni

Inatoka Uk. 18

usafirishaji ndani ya nchi.

Hivi karibuni, serikali imelazimika kutenga bajeti maalum kushughulikia suala hilo.

Waziri wa Ujenzi, Innocent Bashungwa, ameeleza kuwa Rais Samia Suluhu Hassan ameelekeza kutengwa kwa fedha hizo ili kuhakikisha kuwa miundombinu yote iliyoharibiwa na mvua hizo inarejeshwa katika hali yake ya kawaida katika kipindi kifupi kijacho.

Katika mwaka huu wa fedha unaomalizika pia taifa lilikabiliwa na mgao mkubwa wa umeme na hivyo kuathiri uzalishaji wa bidhaa za matumizi ya ndani na kuuza nje.

Mgao huo ulitokana na kupungua kwa maji katika mabwawa ya kuzalisha umeme kutokana na ukame uliokuwa umeikabili nchi hasa kuelekea mwishoni mwa mwaka jana.

Haya yote yalisababisha kupanda kwa bei za bidhaa nchini na hivyo kuongeza gharama za maisha, jambo ambalo linalalamikiwa na watu wengi, wakiwamo wanasiasa wa upinzani ambao wameanzisha maandamano nchini nzima na moja ya jambo wanalolizungumza ni kupanda kwa gharama za maisha.

Mambo mazuri yaja

Hata hivyo, pamoja na matatizo haya, lakini serikali haikuyumba katika utekelezaji wa miradi mikubwa ya maendeleo ingawa kuna baadhi ambayo utekelezaji wake unasuasua.

Ujenzi wa Bwawa la Mwalimu



Mfanyabiashara wa bucha za nyama aliyekutwa eneo la Mbesi, Dar es Salaam, Silvanus Chute, akitoa maoni juu matarajio yake kwa Bajeti Kuu ya Serikali ya Mwaka 2024/2025 inayotarajia kusomwa wiki hii (Picha na Fidelis Felix/Pambazuko).

Nyerere, ambalo litakapokamilika litazalisha megawati 2,115 za umeme, limeanza kuonyesha mafanikio kwani jenereta moja yenye uwezo wa kuzalisha megawati 235 ilianza kufanya kazi miezi michache iliyopita na ndio kwa kiasi kikubwa imesaidia kupunguza makali ya mgawo wa umeme uliokuwa unalikasi taifa.

Kwa upande mwingine, ujenzi wa reli ya kisasa (SGR) nao umeendelea vizuri hasa katika kipande cha Dar es Salaam - Dodoma ambacho kinatarajia kuanza kutoa huduma; kwa kuanzia na safari za Dar es Salaam – Morogoro kabla ya Julai, 2024.

Hata hivyo, kumekuwa na kusuasua kwa ujenzi huo katika awamu nyingine ingawa serikali imekuwa ikihangaika kutafuta fedha kwa ajili ya kuendeleza ujenzi huo.

Barua za Wasomaji

Daladala binafsi ziruhusiwe, tumechoshwa na Mwendokasi

Mhariri,

Kwanza niwapongeze kwa kazi kubwa kinyayoifanya hasa ya kutuhabarisha na kutuelimisha mambo muhimu.

Ninamshukuru Mungu nami kupata nafasi hii ya kutoa dukuduku langu kuhusu usafiri wa mabasi ya Mwendokasi, Dar es Salaam.

Tumekuwa tukiteseka kwa kukaa vituoni tukisubiri mabasi kwa zaidi ya saa tatu. Mfano mimi ninaishi Mbezi na shughuli zangu nafanyia Kariakoo, hivyo kila siku inanilazimu kuamka saa tisa alfajiri kwa ajili kuwahi kukaa kwenye foleni.

Pamoja na kuamka mapema hivyo, unakuta nafika kazini saa tatu, sasa fikiria – je, ningekuwa nachelewa kuamka kazini ningefika saa ngapi?

Na wakati wa jioni nafika kituo cha Gerezani saa kumi jioni, lakini hadi nipate usafiri, unakuta nimekaa zaidi ya saa tatu.

Mbali na hilo la mabasi kuwa machache na kuchelewa kufika kituoni,

tumekuwa tukijazwa kama ng'ombe kiasi kwamba hata kupata hewa ni ngumu na mara kadhaa nimeshuhudia kwa macho yangu watu wakizimia na kutapika.

Kero tunayoipata ni kama usafiri wa bure wakati tunatoa nauli kubwa tu.

Sasa tunajuliwa hivi serikali ambayo tumeipa dhamana, haioni hili na au imeamua tu kufumba macho na kuziba masikio kiasi kwamba haisikii wala kuona changamoto hii?

Miezi chache zilizopita tulimsikia Waziri wa Tamisemi, Mohamed Mchengerwa alitaka Udart na Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka (Dart), kuhakikisha kampuni binafsi inapatikana kabla ya Oktoba mwaka huu.

Baada ya kauli hiyo ya waziri tusikika pia kampuni zaidi ya 30 zikijitosa kuwania zabuni ya uendeshaji wa Udart. Sasa tunashangazwa kwanini wakati mpango huo unaendelea wasingetafuta njia mbadala hata wa kuruhusu daladala binafsi kwa muda?

Joshua John, Mkazi Mbezi Luis.

Kero barabara ya Kitunda-Magole itafutiwe ufumbuzi

Mhariri,

Napenda kuchukua fursa hii kuelezea kuhusu adha ya usafiri tunayoipata sisi wakazi wa maeneo ya Kibeberu na Magole, kutokana na ubovu wa barabara.

Ni miaka mingi sasa sisi wakazi wa maeneo haya tumekuwa tukiishi kwa taabu kutokana na adha ya usafiri, inayosababishwa hasa na ubovu wa barabara.

Tumetoa malalamiko mara kadhaa kuiomba serikali kupitia kwa viongozi wetu, akiwemo mbinge wetu wa Jimbo la

Ukonga, Jerry Silaa, lakini hakuna hatua zozote zinazochukuliwa hivyo kuongeza taabu kwa wakazi wa maeneo haya ambao tunalazimika kutumia gharama kubwa kwa usafiri kwenda kazini na kurudi nyumbani.

Tunaomba mamlaka zinazohusika kulichukulia suala hili kwa uzito wa kipekee kwa kuwa tuna imani na serikali yetu ambayo tunaamini ni sikivu katika suala la kutatua matatizo ya wananchi wake.

Elias Ngoda, Mkazi wa Magole kwa Mpemba, Ukonga, Dar es Salaam.

Tunapokea Barua

Mhariri anapokea barua kutoka kwa wasomaji wake kwa ajili ya kuzichapisha ama kuzitafutia majibu kutoka ofisi za serikali na binafsi. Tuma barua yako kwa njia ya barua-pepe: info@tampa.or.tz au kupitia namba ya simu: 0744 768 263

Wastaafu wasibaguliwe bima ya afya

Na Martin KUHANGA

NI muda sasa tumekuwa tikisikia harakati za serikali kuanzisha mfumo wa bima ya afya kwa wote, lakini jambo hilo zuri limeendelea kusuasua kutokana na sababu zisisokuwa na “nia njema.”

Yaani ni kwamba hadi sasa utaratibu wa kutungwa kwa sheria itakayosimamia mfumo huo unaendelea kupigwa danadana.

Kuwepo nia ya kuanzishwa kwa mfumo huo wa bima ya afya kwa wote ni jambo la kupongezwa, hasa kwa nchi yenye wananchi wake wengi fukara kama Tanzania. Wananchi wake wengi hawana uwezo wa kugharamia matibabu moja kwa moja.

Hata hivyo, inasikitisha kuwa wakati serikali ikiendelea kusuasua kutunga sheria hiyo, wastaafu waliokuwa wanazitumikia taasisi binafsi na kuchangia matibabu kupitia Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) wamekuwa wakinyanyaswa.

Iko hivi; miaka kadhaa iliyopita serikali iliondoa bima ya afya kwa wastaafu kutoka sekta binafsi ambao walikuwa wanachama wa mfuko huo na kuchangia kwa zaidi ya miaka kumi ilhali wastaafu kutoka sekta ya umma ambao walichangia mfuko huo kwa kipindi kama hicho, wakiendelea kunufaika kwa huduma.

Uamuzi huu wa kusikitisha ulifanywa na serikali ya awamu ya tano kupitia marekebisho ya Sheria ya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya, na kuwanyima haki ya kutibiwa maelfu ya wastaafu kutoka sekta binafsi.

K i g e z o

kilichowafanya wastaafu wa sekta ya umma kuendelea kupata huduma hizo ni kimoja tu, kuchangia kwa miaka kumi au zaidi, lakini wale waliotoka sekta binafsi hata kama wametimiza kigezo hicho wameachwa.

Ni dhahiri kuwa kupitishwa kwa marekebisho hayo ya sheria kumeleta ubaguzi kama alivyowahi kusema Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, February 14, 2022, alipokutana na wahariri na waandishi wa habari, katika Ukumbi wa Msekwa, Bungeni jijini Dodoma.

Ileweke kuwa kurejeshwa kwa haki hiyo kwa wastaafu kutoka sekta binafsi kutaongeza - kwa kiasi kikubwa idadi ya wananchi watakaokuwa katika mpango wa Bima ya Afya kwa Wote, kwani wastaafu wa sekta binafsi walio nje ya utaratibu wa matibabu wa NHIF katika kipindi cha zaidi ya miaka mitatu, pamoja na wenza wao, ni wengi.

Wastaafu kutoka sekta binafsi waliochangia NHIF kwa miaka kumi au zaidi wataipunguzia serikali mzigo wa kuwahangaikia katika mpango wa Bima kwa Wote, kwani kimsingi wao wanayo bima ya afya tayari isipokuwa sheria imewaengua.

Ni muhimu kwa wastaafu wa sekta binafsi waliokuwa wanachama wa NHIF kurejeshwa haki ya kutibiwa kwa kuwa nao wamechangia mfuko kwa miaka

Endelea Uk. 22



Wastaafu wakisubiri kupatiwa huduma

Maoni Binafsi

Wastaafu wasibaguliwe bima ya afya

Inatoka Uk. 21

kumi na zaidi, kama wenzao wa sekta ya umma, wanaoendelea kupata matibabu kwa mpango wa bima ya wastaafu.

Ni muhimu kwa wastaafu wa sekta binafsi waliokuwa wanachama wa NHIF kurejeshewa haki ya kutibiwa kwa kuwa wenzao wa sekta binafsi waliostaafu kabla ya kupitishwa kwa marekebisho hayo ya sheria ya kibaguzi, wakiwemo waliostaafu kwa hiari, bado wanaendelea kuipata haki hiyo.

Kwa mfano, mimi nilistaafu Septemba 2021 sina haki ya Bima ya Wastaafu, wakati mwenzangu aliyekuwa astaafu mwaka huu kwa mujibu was sheria, lakini aliamua kustaafu kwa hiari mwaka 2017, ameendelea kutibiwa na mwenzwa wake hadi sasa.

Ni muhimu kwa wastaafu hao kurejeshewa haki ya matibabu kwa kuwa baada ya kustaafu watumishi wote, wakiwemo wa sekta binafsi, wanakuwa hawana kipato cha uhakika kuwawezesha kulipia huduma za matibabu.

Ni muhimu kwa wastaafu hao kurejeshewa haki ya matibabu kwa kuwa baada kutimiza miaka ya kustaafu, 55 au 60, wastaafu wengi hukabiliwa na magonjwa ya uzee na yasiyoambukiza kama kisukari, magonjwa ya moyo, shinikizo la damu na kadhalika, yanayohitaji kupata huduma ya matibabu mara kwa mara.

Iwapo mtu huyu hatosaidiwa katika matibabu kuna uwezekano wa kuongezeka kwa vifo na hata “wagonjwa wa kudumu” ambao ni wastaafu.

Ni muhimu kwa wastaafu hao kurejeshewa haki ya matibabu kwani kwa kuwaondolea haki ya bima ya afya, katika kipindi cha karibu miaka mitatu, wastaafu wengi wameshindwa kupata matibabu kutokana na magonjwa mbalimbali na baadhi yao wamepoteza maisha.

Serikali inayosisitiza usawa wa binadamu haitakiwi kuwabagua watumishi kwa kuzingatia sekta wanazofanyia kazi, kwa sababu wote,



wale wa sekta binafsi na sekta ya umma walifanya kazi moja ya kuliendeleza taifa.

Sasa ni muda muafaka kwa serikali ya inayoongozwa na Rais Samia Suluhu Hassan, kufanya marekebisho katika sheria ya NHIF ili kuondoa tofauti hii ya kibaguzi.

Awali, wakati mifuko ya hifadhi ya jamii ilipokuwa mingi, kiwango cha uchangiaji, mfano katika Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF), ilikuwa asilimia 20 ya mshahara kwa mwezi kwa watumishi kutoka sekta zote, sekta binafsi na sekta ya umma, ingawa watumishi wa umma walisaidiwa na waajiri wao asilimia 15 kati ya zile 20 na huku wale wa sekta binafsi wakitoa asilimia kumi na waajiri wao asilimia kumi.

Mbona serikali hiihii ilirekebisha sheria ili kuondoa utofauti wa kuchangia katika Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) baina ya watumishi wa sekta ya umma na sekta binafsi?

Kwa usikivu wake, serikali ilifanyia marekebisho Sheria ya WCF na kuweka kiwango sawa cha uchangiaji, asilimia 0.5 kwa sekta zote badala ya asilimia moja kwa sekta binafsi na asilimia 0.5 kwa sekta ya umma, wakati kiwango cha fidia kilikuwa kimoja bila kujali kiwango cha uchangiaji.

Mwandishi wa makala haya anapatikana kwa namba 0623545191.

Tuhimize matumizi ya nishati safi ya kupikia

Na Hellen NGOROMERA

KATIKA siku za hivi karibuni, wameonekana baadhi ya wabunge wakigawa majiko ya gesi kwa vikundi vya mama lische na wananchi wengine.

Hatua hiyo sasa inahusishwa na kampeni za kisiasa wakati huu Tanzania ikielekea msimu wa uchaguzi wakati ukweli ni kuwa harakati hizo ni sehemu ya utekelezaji wa mkakati wa miaka kumi wa kitaifa wa matumizi ya nishati safi ya kupikia kuanzia mwaka huu hadi 2034.

Utekelezaji wa mkakati huo unaosimamiwa na Wizara ya Nishati utagarimu shilingi trilioni 4.6 (sawa na dola za Marekani bilioni 1.8) hadi kukamilika kwake.

Pamoja na mambo mengine, mkakati huo una lengo la kuhakikisha jamii inaachana na matumizi na nishati nyingine kupikia kama vile mkaa, kuni na vinyesi vya wanyama.

Inaaminika kuwa kupungua kwa matumizi ya nishati hizo kutapunguza kwa kiasi kikubwa kasi ya kukataji miti Tanzania.

Kwa mujibu wa Rais Samia, matumizi ya nishati hiyo safi kutapunguza tatizo hilo kwa kiasi kikubwa kwani asilimia 90 ya kaya nchini zinatumiya kuni na mkaa.

Moja ya malengo ya mkakati huo ni kuhakikisha kuwa mpango huo unaziingiza asilimia 80 ya kaya katika matumizi ya nishati safi ya kupikia ifikapo mwaka 2034.

Rais Samia ameeleza pia kwamba mkakati huo unasukumwa na ongezeko

la uharibifu wa mazingira, jambo linalosababisha mabadiliko ya tabia nchi na kuleta athari za kiafya, kijamii na kimazingira zinazotokana na matumizi ya nishati isiyo safi ya kupikia.

Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, imekuwa ikibuni na kutekeleza sera na mikakati yenye lengo za kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia pamoja na utunzaji wa mazingira.

Rais Samia amesisitiza kuwa lazima serikali kupitia wizara husika, ikuze na kuvutia uwekezaji zaidi katika uzalishaji wa majiko banifu, umeme na kuhamasisha uzalishaji wa vifaa vya gesi asilia, akibainisha kuwa hatua hizo zitasaidia kupunguza gharama za nishati.

Hili ni jambo la kupongeza, lakini ili mkakati huo ufanikiwe jamii isiishie kwenye kupongeza tu, kwani ili mkakati huo ufanikiwe unahitaji kuungwa mkono na wadau wote wa maendeleo kwa kutekeleza kwa vitendo yaliyomo kwenye mkakati huo.

Mathalan, hisia kuwa kinachofanywa na wabunge wanaogawa majiko ya gesi ni sehemu ya kampeni za kisiasa, isiachwe ikakomaa na kusambaa zaidi, kwani itakwamisha utekelezeaji wa mkakati huo.

Ni wazi kwamba matumizi ya nishati ya kuni na mkaa, yanaendeleza athari nyingi katika jamii, ikiwamo uharibifu wa mazingira na afya.

Kukata miti kwa ajili ya kupata nishati ya kupikia, kumesababisha maeneo mengi kukosa mvua, hivyo kukaribisha upungufu wa chakula.



Biashara ya mkaa ni hatari kwa ustawi wa mazingira

KITUKO CHA DEREVA WA DALADALA



Askari wa Kikosi cha Usalama Barabani, akimkagua dereva wa daladala linalofanya safari zake kati ya Mabibo na Mwananyamala, Dar es Salaam, aliyekuwa amevaa kaptula wakati akiendesha huku suruali aliyopaswa kuvaa akiwa ameitundika kwenye gari kinyume na sheria inayowataka kuhakikisha wanavaa sare muda wote wa kazi. Hapa walikutwa eneo la Kinondoni Studio, Dar es Salaam juzi. (Picha na Fidelis Felix/Pambazuko).

GAZETI hili lilianzishwa 2021, kuandaliwa na kusambazwa na Chama cha Waandishi wa Habari Tanzania (Tampa) na kusajiliwa na Serikali ya Tanzania, kupitia Idara ya Habari (MAELEZO) na kupewa leseni namba - 00000448. Linaendeshwa kwa ushirikiano wa msunguko - kwa kila nchi, wa mwaka mmoja na waandishi wa Tanzania, Kenya, Uganda, DRC na Rwanda.